**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA**

**MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI**

**711** **KISWAHILI**

**Muda: Masaa 3** **Ijumaa, 02rd May 2014 Asubuhi**

---

**Instructions.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali kumi na sit (16).
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na maswali mawili kutoka kila sehem **B** na **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** Zina jumla ya alama **sitini (60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha majibu.

maktaba.tetea.org
TETEA



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii. Kila swali lina alama 4.

1. Tunga sentensi moja kwa kila mojawapo ya viambishi vifuatavyo, na ueleze kazi ya kiambishi hicho katika kila sentensi:
   (a) -li-
   (b) -na-
   (c) -ta-
   (d) -ki-

2. (a) Tofautisha sentensi ambatano na sentensi changamano.
   (b) Andika sentensi moja ya kila aina kwa kutumia viunganishi vinavyofaa.

3. Taja aina mbili za vitenzi ambavyo huonyesha hali ya mhusika na eleza sifa moja ya kila aina uliyotaja.

4. Eleza maana ya nomino za pekee kisha taja mifano miwili na andika sentensi moja kwa mojawapo.

5. Eleza kwa mifano miwili namna vielezi vya wakati hutumika katika sentensi za Kiswahili.

6. (a) Taja ngeli mbili za nomino zinazoonyesha wingi wa viumbe hai.
   (b) Tunga sentensi moja kwa kila ngeli uliyotaja.

7. Eleza maana ya sitiari na tofauti yake na tashbihi kwa kutumia mifano.

8. (a) Eleza maana ya semi.
   (b) Taja semi mbili zinazohimiza maadili na tabia njema.

9. Toa maana ya kazi ya fasihi simulizi na eleza jinsi kazi hiyo inavyochangia malezi ya jamii.

10. Kwa hoja mbili, eleza umuhimu wa kutumia Kiswahili katika kuandika nyaraka rasmi za serikali.

**SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali mawili kutoka sehemu hii. Kila swali lina alama 15.

11. Eleza mchango wa mashairi ya Kiswahili katika kuibua na kujadili matatizo ya kijamii kwa hoja sita.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

12. Kwa hoja sita, eleza sababu zinazowafanya baadhi ya wanafunzi kushindwa kuandika insha kwa ufasaha.

13. Eleza jinsi lugha ya Kiswahili inavyoweza kutumika kama chombo cha ujasiriamali na maendeleo ya kiuchumi kwa hoja sita.

14. Kwa hoja sita, eleza jinsi ambavyo matumizi ya lugha ya Kiswahili katika elimu ya sekondari yanavyoweza kuimarishwa.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu swali moja tu kutoka sehemu hii. Swali hili lina alama 30.

15. Eleza kwa kina mchango wa lugha ya Kiswahili katika kukuza demokrasia nchini Tanzania kwa hoja sita zilizoelezwa vizuri.

16. Jadili namna ya kuendeleza matumizi sahihi ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa Tanzania kwa hoja sita.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org